DEVELOPMENTAL DISABILITIES ADMINISTRATION (DDA)

# Taarifa ya Uhakiki wa Ustahiki wa Umri wa Miaka Ishirini (20)

## Notification of Age Twenty (20) Eligibility Review

JINA LA MTEJA NA ANWANI

JINA NA ANWANI YA MWAKILISHI WA MTEJA

RE: **TAARIFA YA UHAKIKI WA USTAHIKI WA UMRI WA MIAKA ISHIRINI (20)**

Kwa sasa unastahiki kwa ajili ya Idara ya Ulemavu wa Kukua (DDA). Ustahiki wako na DDA sharti uhakikiwe kabla ya siku yako ya kuzaliwa ya miaka ishirini (20) Taarifa tulizonazo huenda zikawa hazitoshi kwako ili kuendelea na ustahiki wako kwa ajili ya DDA chini ya moja ya hali zifuatazo: Ulemavu wa Akili, Ugonjwa wa Kupooza, Kifafa, Ugonjwa wa Akili wa Watoto, au Hali nyingine ya Nyurolojia **au** Hali nyingine Inayofanana na Ulemavu wa Akili. Tumeambatanisha Jedwali ya Nyaraka Zinazotakiwa ili kukujulisha ni taarifa gani inahitajika.

**Je, unahitaji kufanya nini?**

DDA itafurahi kutuma taarifa inayohitajika kwa ajli ya uamuzi huu mwingine. Ikiwa unataka DDA itume taarifa, tafadhali jaza fomu ya idhini iliyoambatanishwa kama ifuatavyo:

1. Andika majina ya sehemu, watoa huduma, na vituo ambavyo tunaweza kuomba taarifa katika fomu ya idhini. Jumuisha taarifa za mawasiliano za watu wote walioorodheshwa kwenye fomu ya idhini.
2. Tia saini na tarehe fomu ya idhini iliyoambatanishwa, na
3. Rejesha fomu hizo kwa DDA.

**Nini kitatokea ikiwa sikujibu ombi hili?**

Tafadhali jibu haraka iwezekanavyo, lakini isiwe zaidi ya siku 90 kabla ya siku yako ya kuzaliwa ya miaka ishirini (20). Ikiwa hatutasikia kutoka kwako hadi mnamo ______________, tutahakiki ustahiki wako kwa kutumia taarifa tulizonazo katika faili lako la mteja. Ikiwa hakuna taarifa za kutosha za kuthibitisha uamuzi wa ustahiki, hivyo ustahiki wako wa DDA utakatishwa mnamo siku yako ya kuzaliwa ya miaka ishirini (20).

Ikiwa una maswali yoyote, wasiliana na:

| JINA | NAMBARI YA SIMU | ANWANI YA BARUA PEPE |
|---|---|---|
| | | |

Nakala ya ulemavu unaoongoza wa kanuni za taifa (WAC 388-823) inapatikana kwa maombi au mtandaoni katika https://www.dshs.wa.gov/dda/consumers-and-families/eligibility.

Viambatanisho: Jedwali la Nyaraka Inayohitajika
Fomu ya idhini (DSHS 14-012)

cc: Faili la mteja

## Jedwali la Nyaraka Inayohitajika

| HALI YA ULEMAVU | UTAMBUZI WA UGONJWA | MTAMBUZI WA UGONJWA | KUMBUKUMBU NYINGINE |
|---|---|---|---|
| Ulemavu wa Akili | Ulemavu wa Akili | Mwanasaikolojia Mwenye Leseni, Mwanasaikolojia wa Shule Aliyethibitishwa na Washington, au mwanasaikolojia mwengine wa Shule aliyethibitishwa na Taasisi ya Taifa ya Wanasaikolojia wa Shule | Ripoti kamili ya Kisaikolojia ikiwemo pointi za Full Scale IQ yenye zaidi ya michepuko miwili yenye kiwango cha chini ya wastani, na pointi za kipimo cha uwezo wa kuendana na hali chenye zaidi ya michepuko miwili yenye kiwango cha chini ya wastani. |
| Ugonjwa wa Kupooza | Ugonjwa wa Kupooza<br>Kuadriplejia<br>Hemiplejia<br>Diplejia | Daktari Mwenye Leseni | Shambulio kabla ya miaka 3, na taarifa inayounga mkono mahitaji ya msaada wa kidaktari wa kila siku na wa moja kwa moja katika sehemu mbili au zaidi (kujipamba, kuoga, kula, kuvaa, kutembea, au mawasiliano). |
| Kifafa | Kifafa au<br>Ugonjwa wa mshtuko wa moyo | Mwananyurolojia Aliyethibitishwa na Bodi | Utambuzi wa ugonjwa kwa mujibu wa rekodi ya kidaktari na kipimo cha nyurolojia, uthibitisho kutoka kwa daktari au mwananyurolojia wa ugonjwa wa shtuko la moyo lisilodhibitika na linaloendelea au kujirudia, na kipimo cha uwezo wa kuendana na hali kinachoonyesha kikomo kikubwa katika utendaji kazi wa kuendana na hali chenye zaidi ya michepuko miwili yenye kiwango cha chini ya wastani. |
| Ugonjwa wa akili wa watoto<br>(kwa DSM-IV) | Tatizo au ugonjwa wa akili wa watoto<br>Kwa 299.00 katika DSM-IV-TR | Mwanasaikolojia Mwenye Leseni, Nesi Mweledi Mwenye Uwezo Aliyesajiliwa (ARNP) anayehusika na ugonjwa wa akili wa watoto au aliyethibitishwa na kituo cha maendeleo au bodi: Mwananyurolojia, Mtaalamu wa Magonjwa ya Akili, au Daktari wa Watoto wa Tabia na Maendeleo | Tathmini kamili kwa DSM-IV inayofikia vigezo vyote vya utambuzi wa ugonjwa, uthibitisho wa kuchelewa au utendaji usio wa kawaida kabla ya umri wa miaka 3 katika jamii, lugha, umahiri wa mawasiliano au mchezo wa ishara au wa kubuni, na kipimo cha uwezo wa kuendana na hali kinachoonyesha kikomo kikubwa katika utendaji kazi wa kuendana na hali chenye zaidi ya michepuko miwili yenye kiwango cha chini ya wastani. |
| Ugonjwa wa Akili wa Watoto wa Spektra<br>(kwa DSM-V) | Ugonjwa wa Akili wa Watoto wa Spektra 299.00<br>Kwa DSM-5 ikiwemo daraja 2 au 3 la ukali katika safu zote mbili | Mwanasaikolojia Mwenye Leseni, Nesi Mweledi Mwenye Uwezo Aliyesajiliwa (ARNP) anayehusika na ugonjwa wa akili wa watoto au aliyethibitishwa na kituo cha maendeleo au bodi: Mwananyurolojia, Mtaalamu wa Magonjwa ya Akili, au Daktari wa Watoto wa Tabia na Maendeleo | Tathmini kamili kwa DSM-IV inayofikia vigezo vyote vya utambuzi wa ugonjwa, uthibitisho wa kuchelewa au utendaji usio wa kawaida kabla ya umri wa miaka 3 katika jamii, lugha, umahiri wa mawasiliano au mchezo wa ishara au wa kubuni, kipimo cha uwezo wa kuendana na hali kinachoonyesha kikomo kikubwa katika utendaji kazi wa kuendana na hali chenye zaidi ya michepuko miwili, na FSIQ yenye mchepuko mmoja au zaidi yenye kiwango cha chini ya wastani – au – kufikia vigezo vyote vya Ugonjwa wa Akili wa Watoto 299.00 kwa DSM-IV. |
| Hali nyingine ya Nyurolojia au Hali nyingine Inayofanana na Ulemavu wa Akili | Magonjwa ya nyurolojia au kromosomu yanayojulikana kwa usababishaji wa upungufu wa uwezo wa akili na uwezo wa kuendana na hali | Daktari Mwenye Leseni | Pointi za Full Scale IQ zenye zaidi ya michepuko yenye kiwango cha 1.5 chini ya wastani, na kipimo cha uwezo wa kuendana na hali kinachoonyesha kikomo kikubwa katika utendaji kazi wa kuendana na hali chenye zaidi ya michepuko miwili yenye kiwango cha chini ya wastani. |

**Zingatia: Fomu hii ni mwongozo wa jumla tu na DDA inaweza kuhitaji taarifa ya ziada au tathmini. Nyaraka hii ni hatua ya kwanza katika uamuzi wa kustahiki. Kustahiki kwa DDA kunaamuliwa kwa mujibu wa Sura ya 388-823 WAC.**